# UCHUNGUZI WA GHASIA ZA WAKATI NA BAADA YA UCHAGUZI MKUU WA OKTOBA 2025

## MUHTASARI WA UCHUNGUZI

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **202**<br>Maeneo yaliyoathirika<br>Mikoa **14**<br>Wilaya **43** | **1,323**<br>Waathirika waliosikilizwa<br><br>**953**<br>Maelezo ya kiapo<br><br>Polisi: **26** | **4,891**<br>Madodoso yaliyopokelewa | **56,000+**<br>Mawasiliano ya kidijitali SMS, WhatsApp, barua pepe | **201**<br>Mijadala ya vikundi<br><br>**3565**<br>Washiriki<br><br>Dar es Salaam:<br>Vikundi **31**<br>Washiriki **1,466**<br><br>Mikoa mingine:<br>Vikundi **170**<br>Washiriki: **2,099** | **450+**<br>Picha Mnato<br><br>**860+**<br>Picha Mjongeo zilizochunguzwa (*Forensic & GIS Analysis*) |

## VYANZO VYA GHASIA (5 VIKUU)

### 1. Kisiasa
- Madai ya Katiba Mpya
- Malalamiko kuhusu Chaguzi
- Migogoro ndani ya vyama

### 2. Kiuchumi
- **Ugumu wa maisha**
- **Ukosefu wa ajira**
- **Kukosekana kwa usawa wa fursa**

### 3. Kijamii
- **Rushwa na ubadhirifu**
- **Utekaji na Kupotea kwa Watu**

  **2023-2025**
  **Walipotea 758**
  **Waliopatikana 503**
  **hawajapatikana 255**

- **Imani ya waanchi kushuka**
- **Uhusiano kati ya wananchi na Jeshi la Polisi**

### 4. Utawala
- **Baadhi ya watendaji (hususan ngazi za chini kuto kushughulikia kero kwa wakati**
- **Mapendekezo ya tume za awali kutotekelezwa**

### 5. Kimataifa
- **Mwenendo ya kijiosiasa**
- **Maslahi ya mataifa mengine nchini Tanzania**

## Vichocheo

### Vichocheo vya Ghasia
- Mitandao ya kijamii: kupanga, kuhamasisha na kuratibu ghasia (kiwango kikubwa zaidi kuliko wakati wowote)
- Kauli za wanasiasa: *"No Reforms No Election"*, *"Oktoba Tunatiki"*, *"Samia Must Go"* n.k. (kauli zaidi ya 12 zilibainishwa)
- Kupanga, kuratibu na kufadhili: vijana walitafutwa, kuhifadhiwa, na kupewa mafunzo ya kushiriki gharia
- Malipo sh. 10,000–50,000 na ahadi za ajira ili kuvutia washiriki
- Baadhi ya wagombea waliokatwa na wanachama

## Malengo

### Malengo ya Ghasia
- Kuzuia au kuvuruga Uchaguzi Mkuu wa 29 Oktoba 2025: Kwa kuharibu vituo vya kupigia kura, kushambulia wasimamizi na wapiga kura, kushambulia na kujeruhi Polisi katika vituo.
- Kushinikiza Serikali: kuleta msongo na kukosa utulivu ili kufikia mabadiliko ya kisiasa
- Kufikisha ujumbe kwa Serikali kuhusu madai na kero za muda mrefu - Malalamiko ya wananchi ya muda mrefu (kiuchumi, kijamii, kisiasa) yalitumiwa na waratibu kama mkakati wa kuwashawishi wananchi, hasa vijana, kushiriki bila kuelewa malengo halisi ya wahusika wakuu.
- Wizi na Uporaji: makundi yalitumia fursa ya ghasia

| | |
|---|---|
| wenye malalamiko katika vyama vyao walitumia ghasia kama fursa na kushiriki chini-chini. | kuiba madukani na maeneo ya biashara |

## Ishara Zilizokuwepo

- Viashiria vya kuvuruga uchaguzi vilikuwepo takribani miezi 6 kabla kupitia mitandao. (TCRA ilitoa taarifa mara kwa mara)
- Uwepo wa vikao vya kupanga na kuratibu ghasia vilivyokuwa vikifanyika mitandaoni (*Club House na Space*)
- Matamko ya baadhi ya wanasiasa, viongozi wa dini, na wanaharakati
- Vijana 500+ walihifadhiwa kwenye majengo na makambi siku 28+, moja ya maeneo ilikuwa umbali mita 10 tu kutoka kituo cha polisi
- Polisi walishtukizwa kwani walijipanga kwa maandamano ya kawaida.

## WAHUSIKA NA MBINU ZILIZOTUMIKA

### Wahusika wa Ghasia

- **Wahusika Wakuu:** waliobuni mipango, kutoa mwelekeo na kusimamia utekelezaji wa ghasia
- **Waratibu:** waliosimamia utekelezaji wa kila hatua, walioweka mawasiliano kati ya wahusika na watekelezaji; hawakuwepo maeneo ya matukio — hali iliyochangia kutokukamatwa kwao
- **Wafadhili:** waliotoa rasilimali fedha, vifaa, na usaidizi wa kimkakati ili kuhakikisha ghasia zinafanyika
- **Watekelezaji:** wengi wao ni wananchi wa kawaida, vijana waliokata tamaa, bodaboda na machinga — walioajiriwa kwa malipo au ahadi; wengi hawakuelewa malengo halisi ya wahusika wakuu

### Mbinu 16 Zilizotumika (Baadhi)

- **Matumizi ya pikipiki:** kupeleka haraka watekelezaji kutoka eneo moja hadi jingine na kutawanya ghasia
- **Mashambulio ya Wakati Mmoja (Dispersal):** kufanya matukio kwa makundi mengi (maeneo 202) na wakati mmoja ili kuwatawanya askari wasiweze kukabiliana kwa urahisi — mbinu hii ilifanikiwa; Polisi walikuwa wamejipanga kwa maandamano ya kawaida, si kwa ghasia za aina hiyo
- **Kufunga Njia/Barabara:** kuweka vizuizi barabarani ili kuzuia usafirishaji wa nguvu za usalama na kuisolate maeneo ya ghasia
- **Kuchoma Vituo vya Mafuta:** kuchoma kwa lengo la kusababisha taharuki, hofu ya umma, na kueneza machafuko haraka
- **Matumizi ya Ishara kama Mawasiliano:** ishara za mkono, rangi na alama maalumu zilitumiwa kati ya watekelezaji kwa usalama bila kuacha ushahidi wa maandishi

## MADHARA YA KIBINADAMU

| | | | |
|---|---|---|---|
| **518**<br>**Jumla ya Vifo**<br>Wanaume 94.6%<br>Raia 96.9%<br>Watoto 21<br>Maiti 480 zilichuliwa na Familia (92.7%) | **90%**<br>**Vifo vya vitu nvenje ncha kali kwa mujibu wa uchambuzi wa kitaalam** | **2,390**<br>Jumla ya Majeruhi<br>**Raia 2,270 (95%) · Askari 120 (5%)** | **219**<br>**Majeraha makubwa**<br>walilazwa hospitali na majeraha madogo waliruhusiwa |

## VIFO KIMKOA

| | | | |
|---|---|---|---|
| **182** Dar es Salaam | **53** Arusha | **20** Shinyanga | **9** Mara |
| **90** Mwanza | **26** Geita | **14** Dodoma | **8** Iringa |
| **80** Mbeya | **20** Songwe | **9** Ruvuma | **5** Pwani |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | **2**<br>Njombe |

| Matokeo ya Uchunguzi wa Maiti | Madhara ya Kijamii na Kisaikolojia |
|---|---|
| **Matokeo ya Uchunguzi wa Kitaalam**<br>• DNA ilifanyika kwa maiti 274 kwa uchunguzi wa kitaalamu<br>**Uchunguzi wa Kitaalamu wa Maiti (Post-Mortem)**<br>• Maiti 219 zilizochunguzwa zote zilitokana na **vifo visivyo vya kawaida**<br>• **Sababu ya moja kwa moja (*Immediate cause*):** kuvuja damu nyingi (147); kujeruhiwa ubongo/brain injury (41); kupaliwa/kukosa hewa (12); kujeruhiwa uti wa mgongo (9); majeraha mbalimbali (5); mshtuko wa moyo (4); sababu haijulikani (1)<br>• **Sababu halisi (*Underlying cause*):** kupigwa risasi vifo **197 (90.0%)**; havikuhusiana na risasi **22 (10%)**<br>• **Maeneo ya majeraha:** mikono na miguu (166 maiti); kifua na tumbo (36 maiti); kichwa na shingo (12 maiti); bila majeraha (4 maiti); moja haikubainishwa — haikuwa na baadhi ya viungo | **Athari za Kijamii na Kisaikolojia**<br>• Msongo wa mawazo, hofu na huzuni miongoni mwa waathirika na familia<br>• Uvunjaji wa mshikamano na kuaminiana ndani ya jamii<br>• Watu 710 waliojitaji msaada wa kisaikolojia walifikiwa na kupatiwa huduma<br>• Waganga na wauguzi kufanya kazi zaidi ya saa 72 bila kupumzika<br>• Madai ya vifo nje ya maeneo yaliyokuwa na ghasia, na maiti ambazo hazijapatikana |

## Madai ya Makaburi ya Halaiki

- Madai ya makaburi ya halaiki Kondo, Kinondoni hayakuthibitishwa na wataalamu wa GIS/ Remote sensing

## MADHARA YA KIUCHUMI

| **Sh. Bilioni 125** | **Sh. Bilioni 89 (71%)** | **Sh. Billion 36 (29%)** | **Sh. Mil. 1.6** |
|---|---|---|---|
| Jumla ya hasara | Sekta Binafsi<br>Vituo vya mafuta, mabasi, magari, maduka, benki | Sekta ya Umma Sh. Bilioni 36 Shule, TRA, DART, TANROADS, TANESCO, TTCL Polisi, Mahakama, | Wajasiriamali wadogo |

## Madhara Zaidi ya Kiuchumi na Kijamii

- Kuvurugika kwa mnyonyoro wa biashara
- Kuathirika kwa Masoko ya fedha
- Kuathirika kwa utalii, usafiri na usafirishaji
- Biashara ziliathirika na kusimama
- Huduma za kujamii kusimama, mfano afya, benki, huduma za kifedha
- Msongo wa mawazo
- Sonona na kiwewe

## MAPENDEKEZO MAKUU

| MUDA MFUPI | MUDA WA KATI | MUDA MREFU |
|---|---|---|
| 1. Matibabu bure kwa walemavu wa ghasia; vifaa saidizi na viungo bandia<br>2. Siku ya Maombolezo ya Kitaifa<br>3. Msaada wa kisaikolojia na tathmini ya haraka (Rapid Assessment)<br>4. Baraza la Taifa la Vijana (Sura 441) liundwe rasmi<br>5. Katiba Mpya ifikapo 2028, Kamati ya Wataalamu ya Katiba iundwe<br>6. Tume ya Maridhiano na Muafaka wa Kitaifa iundwe<br>7. Baraza la Wazee la Ushauri (lisilo rasmi)<br>8. INEC itekeleze sheria 2024, na kuajiri watumishi wake hadi ngazi ya jimbo<br>9. Tume ya Uchunguzi wa Kijinai iundwe (Sura ya 32 ya 2023) kuchunguza vifo vyenye utata, maswala yote ya kijinai (ili kubini wahusika wakuu; waratibu; wafadhili; watekelelezaji)<br>Kuthibitisha na kufuatilia miili ambayo haijaatikana<br>10. Uchunguzi wa kina ufanyike ili kuboresha upelelezi na uwajibikaji kwenye madai ya watu kutekwa na kupotea. | 1. Mifumo ya ukwajibikaji kuimarishwa - watendaji wa ngazi za kati/chini na kushughulikia kero kwa wakati<br>2. Utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai na Vikosi kazi vya awali<br>3. Mfumo wa ajira kwa sifa (merit-based) — kutenganisha siasa na utumishi<br>4. Kuimarisha usalama wa mipaka — vipenyo vingi<br>5. Kurejesha mfumo wa nyumba kumi kisheria<br>6. Mfumo wa usimamizi wa fursa za vijana (mikopo, ajira, miradi ya serikali)<br>7. Mapitio ya bajeti — rasilimali zaidi kwa uwezeshaji wananchi kiuchumi<br>8. Kupanua maeneo katika Sheria ya Usimamizi wa Maafa (Sura 242) | 1. Jeshi la Polisi libuni mkakati wa kujenga upya uhusiano na jamii<br>2. Serikali na vyombo vya dola vizingatie mfumo wa demokrasia katika mfumo wa vyama vingi<br>3. Maadili ya viongozi yasimamiwe kwa karibu — rushwa na ufisadi vidhibitiwe<br>4. Majadiliano baina ya dini — mipaka kati ya dini na siasa ibainishwe<br>5. JKT iwe sharti la lazima kwa wahitimu wote wa kidato cha sita<br>6. Makazi maalumu (barracks) kwa askari ili epuka mgongano wa maslahi |